



## **TANGAZO LA MAHAFALI YA 19 YA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)**

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kinawatangazia wahitimu wote wa mwaka wa masomo wa 2022/2023 wa Kampasi zote pamoja na wananchi wote kwa jumla kwamba, mahafali ya Kumi na Tisa (19) ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar yatafanyika siku ya Alkhamis ya tarehe 28 Disemba, 2023 katika ukumbi wa Dkt. Ali Mohamed Shein ulioko Kampasi ya Tunguu kuanzia 2:30 asubuhi.

Mazoezi ya mahafali (*rehearsal*) yatafanyika Jumatano ya tarehe 27 Disemba, 2023 kuanzia saa 2:30 za asubuhi katika eneo yatakapofanyika mahafali hayo. Wahitimu wote watakaoshiriki katika mahafali ni lazima washiriki katika mazoezi haya katika siku na wakati uliotajwa.

Aidha wahitimu watalazimika kuthibitisha ushiriki wao katika kampasi ya tunguu kuanzia siku ya Jumatatu ya tarehe 18 Disemba, 2023. Uthibitisho huo unatakiwa uambatane na malipo ya joho la mahafali kwa kutumia namba ya malipo (control number) ambazo zitatolewa kupitia ofisi za wahasibu. Ithibati ya malipo ya joho itafanyika kwa uhakiki wa ankara ya malipo itakayowasilishwa..

Majoho ya mahafali yatatolewa katika Kampasi ya Tunguu kuanzia siku ya Jumatatu ya tarehe 18 Disemba, 2023 saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.00 Alasiri na mwisho wa kutolewa ni siku ya mazoezi ya mahafali. Malipo ya kukodi joho ni Tsh. 25,000/- ambazo zitalipwa kupitia akaunti ya SUZA ya Benki ya Watu wa Zanzibar ama wakala wa PBZ.

Wahitimu wanapaswa kurudisha majoho si zaidi ya tarehe 2 Januari 2023. Faini ya TZS. 5,000 itatozwa kwa kila siku itakayozidi baada ya siku ya mwisho iliyopangwa. Inasisitizwa kuwa **wahitimu watajigharamia wenyewe gharama za chakula na malazi kwa kipindi chote cha maandalizi na mahafali. Mtu yoyote hataruhusiwa kuingia kwenye ukumbi wa mahafali baada ya kuingia Mheshimiwa Mkuu wa Chuo. Aidha siku ya mahafali washiriki wanatakiwa wawe wamekaa katika nafasi walizopangiwa ifikapo saa 2.30 asubuhi.**

**WANANCHI WOTE MNAALIKWA KUSHIRIKI NA KILA ATAKAYESIKIA  
TANGAZO HILI ANAOMBWA AMUARIFU MWENZIWE**

***IMETOLEWA NA OFISI YA NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – TAALUMA,  
UTAFITI NA USHAURI ELEKEZI  
CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)***